# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA NISHATI

### WAKALA WA NISHATI VIJIJINI

Energising Rural Transformation

**TANGAZO LA FURSA ZA MIKOPO NAFUU YA UWEZESHAJI WA UJENZI NA UENDESHAJI WA VITUO VIDOGO VYA BIDHAA ZA MAFUTA (PETROLI NA DIZELI) VIJIJINI**

**TAREHE YA KUTANGAZA: 24/5/2023**

## 1. UTANGULIZI

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ulianzishwa kwa Sheria ya Nishati Vijijini, Na. 8 ya Mwaka 2005 na kuanza rasmi kutekeleza majukumu yake Mwezi Oktoba 2007. Wakala wa Nishati Vijijini unatekeleza Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 ambapo awali Wakala ulikuwa unatekeleza Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003 iliyokuwepo wakati wa kuanzishwa kwake. Sheria ya Nishati Vijijini pia ilianzisha Bodi ya Nishati Vijijini pamoja na Mfuko wa Nishati Vijijini.

Wakala wa Nishati Vijijii ni Taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Nishati, yenye jukumu la kuwezesha upatikanaji wa nishati bora vijijini na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo kwa lengo la kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi vijijini. Wakala wa Nishati Vijijini, kupitia Wizara ya Nishati hufanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wabia wa Maendeleo, Idara na Mashirika mbalimbali ya Serikali.

Katika kuhakikisha nishati bora na salama maeneo ya vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini, umeendelea kutekeleza majukumu yake ukijikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na mafanikio makubwa yameonekana. Wakala wa Nishati Vijijini pia unatekeleza miradi mbalimbali ya Nishati ya kupikia. Katika kuongeza upatikanaji wa nishati vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini pia una wajibu wa kuhakikisha nishati ya mafuta inayopatikana vijijini ni safi na salama.

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imedhamiria kuanzisha mpango wa kuwezesha ujenzi wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu vya bidhaa za mafuta (petroli na dizeli) maeneo ya vijijini ili kuondosha madhara yatokanayo na njia zisizo salama. Madhara hayo ni pamoja na:-

a) Gharama kubwa za upatikanaji wa bidhaa hizo maeneo ya vijijini tofauti na bei elekezi;
b) Gharama kubwa za usafiri hasa maeneo ya vijijini;
c) Kuadimika kwa bidhaa hizo maeneo ya vijijini;
d) Uuzaji na uhifadhi wa bidhaa za mafuta usio safi na salama (mapipa na madumu ya plastiki ndani ya nyumba) kwa matumizi ya vyombo vya moto;
e) Milipuko ya moto ambayo inaweza kugharimu maisha ya wananchi na hivyo kupunguza nguvu kazi ya Taifa;
f) Uharibifu wa mazingira unaotokana na bidhaa hizo kumwagika maeneo mbalimbali kwa sababu ya uhifadhi usiofaa;
g) Kuikosesha Serikali mapato ambayo wauzaji wa mafuta (petroli na dizeli) hawalipi kodi na tozo mbalimbali; na

h) Kuathiri afya kutokana na kuvuta hewa isiyo safi na salama kwa sababu ya kuhifadhi bidhaa hizo ndani ya nyumba.

Kwa kutambua hali hiyo, na kwa kuzingatia moja ya malengo ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015, ni wajibu wa Wakala kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati na kwa bei nafuu katika maeneo yote ya nchi kwa njia iliyo salama. Wakala wa Nishati Vijijini umetenga fedha kwa ajili ya kutoa mkopo nafuu kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo vya kuuzia bidhaa za mafuta (petroli na dizeli) vijijini. Mkopo huu utasaidia uwezeshaji wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu maeneo ya vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya mafuta kwa gharama nafuu, kwa njia salama, na isiyo na madhara kwa mazingira.

Wakala unakaribisha waomabaji wenye vigezo kuomba mkopo ili kuwezesha ujenzi na uendeshaji wa vituo vipya vidogo vya gharama nafuu maeneo ya vijijini.

## 2. LENGO KUU LA MRADI

Lengo la mradi huu ni kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo nafuu kwa waendelezaji waliokidhi vigezo vya kupata mkopo wa kujenga na kuendesha vituo vidogo vya mafuta (petroli na dizeli) katika maeneo ya vijijini ya Tanzania Bara.

## 3. FAIDA ZA MRADI

Utekelezaji wa mradi huu una faida zifuatazo: -

a) Kuongeza upatikanaji wa bidhaa za mafuta (petroli na dizeli) vijijini na kwa bei nafuu;
b) Kulinda mazingira na usalama wa jamii na mali zao;
c) Kuondoa madhara ya kiafya yatokanayo na uvutaji wa hewa isiyo safi na salama;
d) Kuondoa uhifadhi wa mafuta usio safi na salama maeneo ya vijijini;
e) Kuepusha uharibifu wa vyombo vya moto vilivyoko maeneo ya vijijini;
f) Kupunguza gharama za usafiri maeneo ya vijijini; na
g) Kuongeza mapato ya Serikali kutokana na uuzaji wa mafuta (petroli na dizeli) uliozingatia taratibu zilizopo.

## 4. UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI

Utaratibu utakaotumika kutekeleza mradi huu umeainishwa katika mwongozo wa mradi ambao unapatikana kupitia tovuti ya Wakala ambayo ni ***www.rea.go.tz***. Mwongozo huo umeainisha vigezo vitakavyotumika kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuleta matokeo chanya yanayokusudiwa na Serikali. Mwongozo umeainisha namna ya kuomba mkopo, uidhinishwaji wa mkopo, vigezo vya mwombaji vya kiufundi na vya kifedha na masharti ya mkopo.

## 5. NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Mwombaji atatakiwa kujaza fomu maalum ambayo inapatikana pia katika tovuti ya Wakala wa Nishati Vijijini ***(www.rea.go.tz).*** Maombi yaliyokamilika pamoja na viambatisho vyake yawasilishwe kwa njia ya zifuatazo: -

a) Anuani ya posta ya Wakala wa Nishati Vijijini ambayo ni:

Mkurugenzi Mkuu,
Wakala wa Nishati Vijijini – REA,
Jengo la PSSSF, Ghorofa ya 7,
Barabara ya Makole,
S. L. P 2153,
**Dodoma, Tanzania.**

Juu ya bahasha baada ya anuani ya Wakala iandikwe **'Maombi ya Mkopo kwa Ajili ya Ujenzi wa Vituo vya Mafuta Vijijini'**

b) Barua pepe:- vituovyamafuta@rea.go.tz

Mwisho wa kuwasilisha maombi ya mkopo ni tarehe **25/8/2023** saa **tisa na nusu alasiri.**

Kwa maelezo zaidi kutoka kwa Wakala wa Nishati Vijijini yawasilishwe kupitia barua pepe iliyotajwa hapo juu na kwa njia ya simu wasiliana na wafuatao:

**Jina:** Michael J. Kyessi
**Namba ya simu**: 0686 033243
**Barua pepe**: mkyessi@rea.go.tz

**Jina:** Deusdedit E. Malulu
**Namba ya simu**: 0788 416284
**Barua pepe:** dmalulu@rea.go.tz

Imetolewa na: -

Mkurugenzi Mkuu,
Wakala wa Nishati Vijijini – REA,
Jengo la PSSSF, Ghorofa ya 7,
Barabara ya Makole,
S. L. P 2153,
**Dodoma, Tanzania.**